AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA
UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

**BARAZA KUU**
**Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Nne**
**15 Januari - 15 Februari 2024**
**Addis Ababa, ETHIOPIA**

**EX.CL/1487(XLIV)Rev.2**
Lugha chanzi: Kiingereza

# RIPOTI YA MKUTANO WA TUME KUHUSU UENDESHAJI WA MFUKO WA AMANI WA UMOJA WA AFRIKA

## UTANGULIZI

1. Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika (AUPF) Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika (AUPF) unatumika kama ushuhuda usio wa kawaida wa dhamira isiyoyumba na maendeleo makubwa ya Afrika katika kufanikisha maadli yake ya kimfano. Ushuhuda wa 'Umoja wa nia' wa Afrika, dhihirisho la sasa la maadili ya waasisi wetu ya umajumui wa Afrika, ni taasisi ambayo imeundwa kwa uangalifu ili kutumia uwezo kamili wa rasilimali zetu za pamoja ili kuendeleza maendeleo yetu wenyewe na kuendeleza jitihada zetu za kuleta amani. Mfuko huu uliundwa Juni 1993, kabla ya AU yenyewe, na kuhuishwa kupitia mchakato wa mageuzi kwa miundo ya utawala na sheria za kifedha zilizoimarishwa ambao uliungwa mkono na Uamuzi wa Mkutano Mkuu wa AU *Decision 605 (XXVII)* wa tarehe 18 Julai 2016. Mfuko wa Amani ni chombo muhimu cha uendeshaji katika kutimiza mamlaka ya AU ya kufanikisha amani na usalama ndani ya bara hili na kujenga Afrika iliyoungana na yenye ustawi.

2. Msingi wa kisheria wa AUPF unaweza kupatikana katika Ibara ya 21 ya Itifaki inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama (PSC) la Umoja wa Afrika, ambayo ilitoa wito wa kuanzishwa kwa mfuko ili kutoa rasilimali muhimu za kifedha kwa ajili ya kazi maalumu za kusaidia kuleta amani na shughuli nyingine za uendeshaji zinazohusiana na amani na usalama barani Afrika. Leo, Mfuko wa Amani unatarajiwa kuchukua jukumu muhimu katika Muundo wa Amani na Usalama wa Afrika (APSA).

## MUUNDO WA UTAWALA NA USIMAMIZI

3. Mfuko wa Amani umeanzishwa rasmi kwa kuimarishwa kwa utawala, uangalizi, uwajibikaji, kanuni za uaminifu, na taratibu kwa kuzingatia umiliki wa kimsingi wa Kiafrika wenye msaada wa ushauri ulioimarishwa na uangalizi kutoka kwa wabia wanaochangia. Utawala wa sasa wa Mfuko wa Amani ambao unakaribia kufanya kazi kikamilifu umeundwa kama ifuatavyo:

- **Baraza la Amani na Usalama (PSC)** - Maamuzi ya PSC ya AU kuhusu upatanishi na diplomasia ya kuzuia migogoro pamoja na kuongoza vipaumbele vya ufadhili vya Mfuko wa Amani.

- **Bodi ya Wadhamini (BoT)** - Bodi ya Wadhamini ina nafasi ya uwajibikaji wa uaminifu kwa Mfuko na kwa hivyo ina jukumu la usimamizi na ufuatiliaji wa Mfuko wa Amani kwa Vyombo vya Sera vya AU. BoT inajumuisha wajumbe watano wa Afrika wanaowakilisha Kanda tano za AU na wajumbe wawili kutoka wabia wa kimataifa wa kimkakati wa AU: Umoja wa Ulaya na Umoja wa Mataifa. Mwaka 2023 wajumbe wa BoT walifanya mikutano ya kawaida minne (4) na kufanya mikutano maalumu miwili (2), na mikutano miwili (2) ya kamati ua ukaguzi.

- **Kamati Tendaji ya Usimamizi (EMC)** – Mwenyekiti wa AUC, Makamu Mwenyekiti, na Kamishna wa Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama, ni wajumbe wa EMC. Mwenyekiti huongoza EMC, na Mkurugenzi wa

Sekretarieti ya Mfuko wa Amani atashiriki (yaani, kutopiga kura). Kazi ya msingi ya EMC ni kutekeleza usimamizi wa kiutendaji na uangalizi wa Mfuko wa Amani na kuwajibika kuongoza shughuli zake.

- **M(wa)simamizi wa Mfuko** – Hufanya usimamizi, uwekezaji, uhasibu na utoaji taarifa wa mfuko kwa niaba ya Sekretarieti ya Mfuko wa Amani. Baada ya mchakato mkali wa zabuni, BoT iliteua wasimamizi wawili wa mfuko ambao ni *Old Mutual Investment Group* kutoka Afrika Kusini na *Sanlam Investments East Africa* kutoka Kenya. Fedha zote za Mfuko wa Amani wa AU zimehamishwa na ziko chini ya usimamizi wa uwekezaji wa wasimamizi hawa wa mfuko. Kwa kuteua wasimamizi huru wa mfuko, AU imehakikisha utendakazi bora katika usimamizi wa mfuko wa kimataifa, unaoweka malengo ya uwekezaji ya uhifadhi wa mtaji, ukwasi na ukuaji wa Mfuko wa Amani na kukuza uendelevu wa kifedha wa Mfuko wa Amani.

- **Sekretarieti ya Mfuko wa Amani** - Sekretarieti ina jukumu la usimamizi wa jumla wa Mfuko wa Amani.

- **Kikundi Huru cha Tathmini (IEG)** - IEG ni kikundi kisicho na upendeleo na huru cha wataalamu walioteuliwa na BoT kuhusu mapendekezo ya EMC ambalo lina jukumu la kufanya mapitio huru ya kiufundi ya athari ya kiutendaji na kiuendeshaji ya Mfuko wa Amani kwa msingi wa muda mfupi.

4. Chini ya mamlaka ya Afisa Mkuu wa Udhibiti (Makamu Mwenyekiti), Sekretarieti ya Mfuko wa Amani inashughulikia shughuli za kila siku za Mfuko huo kwa kushirikiana kwa karibu na Afisa Mkuu wa Fedha (Kurugenzi ya Fedha katika AUC). Kwa sasa, Mkurugenzi wa Mfuko wa Amani ameshika madaraka na anaunda Sekretarieti.

5. Mamlaka ya Bodi ya Wadhamini yamehuishwa. Mwakilishi kutoka kanda ya kaskazini ameteuliwa na mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika kukamilisha muundo wa Bodi. Hata hivyo, mjumbe wa bodi yetu ya Kanda ya Magharibi amejiuzulu hivi karibuni na Mwenyekiti mapema atamteua mbadala kutoka eneo hilo.

6. Sekretarieti imeandaa na kuwasilisha Hadidu za Rejea za Kikundi Huru cha Tathmini (IEG), chombo pekee cha usimamizi kilichosalia ambacho hakijatumiwa, kwa Bodi ya Wadhamini ambayo imekiidhinisha. Sekretarieti itaanza uteuzi wa wajumbe wa Kikundi hiki kupitia Watu Mashuhuri wa Afrika wanaosimamia ajira ya Makamishna wa AU. Jambo hili litachangia kuwa na uwazi ulioimarishwa kufuatia uamuzi wa Baraza Kuu (EC) wa kukamilisha mchakato wa kuajiri wa IXG kupitia Watu Mashuhuri kama ilivyoainishwa kwenye ripoti ya uamuzi wa kamati ndogo za PRC. Sekretarieti inatarajia kutumia IEG kwa mwaka 2024.

7. Kama sehemu ya uendeshaji wa mfuko wa Amani nyaraka muhimu za sera zifuatazo zimetayarishwa na kuidhinishwa.

8. Mfuko wa Amani una sura maalum katika Kanuni za Fedha za AU zilizoidhinishwa mwezi Februari 2022. Mfuko wa Amani umeandaa mwongozo wa kina wa fedha kwa ajili

ya uendeshaji wake na usimamizi wa fedha.

9. Kwa kuzingatia Uamuzi wa Baraza Kuu *EX.CL/ Dec.1218 (XLIII)* Aya ya F.18 ya Julai 2023 na Kanuni ya 48 ya Kanuni za Fedha za AU, Sekretarieti ya Mfuko wa Amani imeandaa "taratibu za kutumia na kujaza tena Mfuko wa Amani wa AU, na Sera yake ya Usimamizi wa Hatari na Orodha ya Hatari. Nyaraka zote mbili ziko katika hatua ya rasimu.

## UTENDAJI WA MSIMAMIZI WA MFUKO

10. Mnamo mwaka 2023, Sekretarieti ya Mfuko wa Amani kwa kushauriana na wasimamizi wa mfuko na F15 ilifanya mapitio ya kina ya miongozo ya uwekezaji ya Mfuko wa Amani. Mambo matatu muhimu ya marekebisho yaliainishwa ambayo ni pamoja na hatua zinazohusiana na ongezeko la uwezo wa kuwekeza katika hatifungani za serikali, matumizi ya bidhaa nyambuo (*derivatives*) kwa madhumuni ya usimamizi bora wa uwekezaji na kuongezeka kwa muda wa ukwasi katika uwekezaji mkuu wa mfuko ili kuruhusu uwekezaji tofauti tofauti.

11. Sekretarieti ya Mfuko wa Amani ilifanya mapitio yake ya kwanza ya utendaji kazi wa wasimamizi wa mfuko mwezi Agosti 2023, ambapo muda wa uwekezaji na wasimamizi wa fedha ulikuwa umefikia mwaka wake wa kwanza. Riba iliyopatikana kutoka kwa *Sanlam investments* ilikuwa imezidi ile ya *Old Mutual Investment Group.* Hivyo Bodi ya Wadhamini ilitenga tena asilimia ya Mfuko wa Amani inayosimamiwa na *Sanlam Investments*.

12. Matarajio kwa mwaka 2024 ni kwamba wasimamizi wa mfuko watapata dola za Marekani milioni 15 -19 katika faida iliyopatikana.

## UFADHILI WA MFUKO WA AMANI

13. Malengo ya kifedha ya Mfuko wa Amani uliohuishwa ni kufikia lengo la dola za Marekani milioni 400 kama ufadhili wa mwanzo kutoka michango ya Nchi Wanachama na kuvutia ufadhili kutoka nje.

14. Mfuko wa Akiba wa Migogoro *(Crisis Reserve Facility*) (CRF), kama sehemu ya Mfuko wa Amani, hutoa ufadhili wa haraka wa kukabiliana na dharura kwa migogoro ya amani na usalama barani Afrika. CRF inaipatia taasisi hiyo uhuru wa kushughulikia majanga ya haraka ambayo huzuka bila tahadhari ya kutosha.

15. Mwezi Februari 2023, Baraza Kuu, kupitia Uamuzi *Ex.CL/Dec.1213 (XLII)* liliidhinisha michango iliyopitiwa ambayo ilisababisha nakisi ya dola za Marekani 28,136,379.12. Baraza Kuu katika Uamuzi huohuo 1213, liliidhinisha pendekezo la kutafuta michango ya hiari kutoka Nchi Wanachama na michango kutoka sekta binafsi ya Afrika ili kujaza upungufu huo.

16. Kiwango cha makusanyo kufikia tarehe 31 Desemba 2023 ni 84% ya ufadhili wote wa dola milioni 400 na 90% ya 371,868,538 ambazo ni mchango uliotathminiwa wa nchi wanachama kwa Mfuko wa Amani kufuatia kupitishwa kwa pendekezo la Kanda ya Kaskazini.

17. Pamoja na jumla ya Dola za Marekani 334,582,565.47 zilizokusanywa kutoka nchi wanachama kulingana na kipimo cha tathmini iliyopelekwa hadi 2023 na pendekezo la Kanda ya Kaskazini, Mfuko wa Amani pia unachangia kiasi cha dola za Marekani 56,735,675.5, ambacho kinaundwa na:

- Mapato kutoka kwa Mfuko wa Amani wa Urithi: **Dola za Marekani 25,032,053.75**
- Riba iliyopatikana kwa uwekezaji kwenye amana isiyobadilika: **Dola za Marekani 16,904,183.52**
- Riba inayopatikana kutoka kwa wasimamizi wa mfuko: **Dola za Marekani 14,299,794.78**
- Mchango wa hiari kutoka Jamhuri ya Senegal: **Dola za Marekani 499,643.45**
- Fedha zilizotolewa (CRF): **Dola za Marekani milioni 7**

18. Itambulike kuwa nchi wanachama thelathini na wanne (34) wamelipa 100% ya mchango uliotathminiwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2023.

19. Kwa hiyo, salio la jumla la Mfuko wa Amani hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2023 ni dola za Marekani 384,318.240.97 ikiwemo jumla ya faida iliyopatikana na mapato kutoka kwenye Mfuko wa Urithi wa AU.

## UMUHIMU WA MAJARIBIO YA MATUMIZI YA MFUKO WA AMANI

20. Maendeleo mazuri yamepatikana katika kutekeleza vipengele vya kitaasisi vya Mfuko wa Amani. Kwa hivyo, masharti ya chini zaidi yanafikiwa ili kuchukua hatua inayofuata ya majaribio ya Mfuko. Bara letu limekumbwa na hali ngumu sana ambazo zilitoa changamoto kwa uwezo wa Tume wa kujibu kama inavyopaswa na wakati inayopaswa. Changamoto hizi zilithibitisha kufaa kwa wazo la kutumia Mfuko wa Amani ili kukidhi mahitaji hayo na yanayofanana na hayo. PSC iliombwa sana ushauri kuhusu hilo. Wawakilishi wa Kamati Tendaji inayoundwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Masuala ya Siasa, Amani na Usalama (PAPS), kwa kushauriana na Mwakilishi Mkuu wa AU kuhusu Ufadhili wa Umoja wa Afrika na Mfuko wa Amani, wameainisha vipaumbele vya matumizi ya Mfuko huo.

21. Baadaye, maeneo 15 ya kipaumbele ya kimkakati yaliainishwa kwa ajili ya matumizi ya Mfuko, ambayo ni dola za Marekani milioni 5, yalipitiwa upya na kukubaliwa na Kamati ya Wataalamu ya PSC (CoE) na kupendekezwa na BoT kwa Kamati Ndogo ya PRC. Mnamo tarehe 20 Juni 2023, maeneo ya kipaumbele ya Kimkakati pia yaliwasilishwa kwa PSC wakati wa mkutano wake Usio Rasmi wa 8 wa Mashauriano na Kamishna wa Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama. Aidha, Idara ya PAPS imeandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya pendekezo la bajeti kwa ajili ya matumizi ya majaribio ya Mfuko wa Amani. Dola milioni 5 zilizopendekezwa kwa ajili ya miradi ya

majaribio zinaidhinishwa na PRC. Baadaye kikao kifupi kuhusu utekelezaji wa miradi ya majaribio kwa RECs na REMs kinapangwa kufanyika mapema mwezi Februari.

## MFUKO WA AKIBA WA MIGOGORO

22. Mfuko wa Akiba wa Migogoro (CRF) ni Mfuko wa Dhamana Usiopungua unaotabiriwa katika Ibara ya 21 ya itifaki ya PSC ambao ni sehemu ya taratibu za ufadhili za Mfuko wa Amani. Kimsingi, CRF ingeipatia AU uhuru wa kushughulikia majanga ya haraka ambayo yanazuka bila tahadhari ya kutosha.

23. Ikumbukwe kwamba PSC katika mkutano wake wa 1153 uliofanyika tarehe 12 Mei 2023, katika Ngazi ya Mawaziri, ilipitisha taarifa [PSC/MIN/COMM.1153(2023)], ambapo iliamuliwa kuongeza ukomo wa CRF kwa mwaka 2023 na kifungu hichohicho kutenga milioni 10 kwa mwaka 2024; ili kuwezesha AU kushughulikia kwa haraka na kwa ufanisi changamoto za dharura za amani na usalama katika ndani ya Bara. Kuhusiana na hili, Baraza liliiomba Tume ya AU kuwasilisha uamuzi huu kwa vyombo vya Sera husika vya AU kwa kuzingatia Kanuni za Fedha za AU.

24. Kufuatia uamuzi wa PSC, CPAPS ilitoa taarifa kwa BOT, ambayo iliidhinisha kiasi cha ziada kwa ajili ya CRF. Taarifa kama hiyo ilitolewa kwenye Kikao cha Pamoja cha Kamati Ndogo ya PRC ya Usimamizi na Uratibu wa Jumla kuhusu Masuala ya Utawala, Bajeti na Fedha, na Wataalamu wa Kamati ya Mawaziri wa Fedha Kumi na Watano (F15).

25. Kwa kuzingatia pendekezo la PRC, kulikuwa na ongezeko la kiwango cha Mfuko wa Akiba wa Migogoro kutoka dola za Marekani milioni 5 hadi milioni 7 kwa mwaka 2023 na pendekezo la dola milioni 10 kwa ajili ya CRF kwa mwaka 2024 limefanyika. Kiwango hiki cha CRF cha 2023 na 2024 kimeidhinishwa na vyombo vya sera vya AU. Madhumuni ya ongezeko hilo ni kuhakikisha mwitikio wa haraka wa AU wakati wa awamu ya kuanza kwa shughuli mpya za kusaidia kuleta amani na upatanishi na diplomasia ya kuzuia migogoro; na kukidhi mahitaji yoyote ya matumizi yasiyotarajiwa na yasiyo ya kawaida yanayohusiana na shughuli za Usaidizi wa kuleta Amani na upatanishi na diplomasia ya kuzuia migogoro. Kwa mujibu wa uamuzi wa EMC, malipo matano ya jumla ya dola za Marekani milioni 6.5 yalitolewa kupitia Idara ya Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama (PAPS) mwaka 2023:

- Dola za Marekani milioni 2 : Kikosi cha kikanda cha EAC katika DRC Mashariki
- Dola za Marekani milioni 2 : Upungufu wa ATMIS
- Dola za Marekani milioni 1.5 kwa ajili ya usitishaji kiufundi wa awamu ya II ya Ujumbe wa Mpito wa Umoja wa Afrika nchini Somalia (ATMIS)
- Dola za Marekani milioni 1 kwa ajili ya upokonyaji silaha, uondoaji askari na uundaji tena katika Ethiopia ya Kaskazini, ukanda wa Tigray ili kuimarisha mchakato wa kuleta Amani wa Pretoria Dola za Marekani 500,000 kwa ajili ya Sudan (hazijatolewa bado)

## UKUSANYAJI WA RASILIMALI

26. Sekretarieti ya Mfuko wa Amani imefanya kazi kwa bidii ili kupata rasilimali endelevu, zinazotabirika, na za kutosha kulingana na mamlaka yake ya kuanzishwa. Ili kufanikisha hili, Sekretarieti ya Mfuko wa Amani ilifanya zoezi la kina la kuainisha wadau, kuainisha wahusika wakuu wanaohusika kwenye Mfuko wa Amani wa AU. Wadau hawa ni pamoja na Nchi Wanachama, taasisi za fedha, vituo vya maarifa, mashirika ya hisani, wabia wa maendeleo, na balozi.

27. Mfuko wa Amani unapanga kimkakati tukio la kukusanya rasilimali kando ya Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka wa 2024, ambapo sekta binafsi pia itashiriki. Ili kukuza ufahamu, majukwaa yaliyopo kama vile Mkutano Mkuu kati ya Umoja wa Ulaya na Afrika, FOCAC na mengineyo yatatumiwa katika mwaka wote wa 2024.

28. Sekretarieti ya Mfuko wa Amani wa AU lazima ihakikishe kwamba Mfuko wa Amani wa AU unabakia kuwa mada kuu katika majukwaa yote husika. EMC na BoT zitakuwa na jukumu muhimu katika kuongoza jitihada za kukusanya rasilimali. Zaidi ya hayo, Sekretarieti ya Mfuko wa Amani inachunguza ushirikiano na Watu Binafsi Wenye Utajiri mkubwa (HNWIs) na makampuni kote Afrika na wanadiaspora ili kuhakikisha uwakilishi unakuwepo kutoka kanda zote katika jitihada za kukusanya rasilimali. Kuzingatia ujuzi kutoka kwenye uzoefu wa awali wa ukusanyaji wa rasilimali wakati wa vita dhidi ya Ebola na UVIKO-19 kunaweza kuboreshwa zaidi kwa ajili ya kuleta mafanikio.

## MPANGO ULIOPENDEKEZWA KUENDELEA KWA MWAKA 2024:

29. Tume ilitoa mapendekezo yafuatayo:

(i) Kwa kuzingatia uamuzi wa EMC, Sekretarieti ya Mfuko wa Amani itaendeleza jitihada zake zote katika kukusanya rasilimali za ziada kupitia michango ya hiari ya nchi wanachama, kwa kushirikiana na wabia, sekta binafsi, watu binafsi wenye utajiri mkubwa na wananchi wa bara letu. Jitihada za pamoja za nchi wanachama na wadau wote zitakuwa muhimu kwa mafanikio ya jitihada hizi;

(ii) Jitihada zinapaswa kufanywa ili kutimiza ahadi kwa nchi wanachama ambazo hazijatimiza ahadi zao kwa Mfuko wa Amani;

(iii) Kuendesha Kikundi Huru cha Tathmini kutakuwa mojawapo ya vipaumbele muhimu vya tume.

(iv) Mkutano Mkuu wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali kukasimisha kwa Baraza Kuu mamlaka ya kujadili na kuidhinisha ukomo uliorekebishwa wa CRF kwa mwaka wa fedha 2025 wakati wa Mkutano wake wa Kawaida utakaofanyika mwezi Juni/Julai 2024.

(v) Kukamilisha taratibu za kutumia na kuujaza tena Mfuko wa Amani na kuwasilisha kwa Baraza Kuu, kupitia njia sahihi, wakati wa Mkutano wake wa Kawaida wa 45 utakaofanyika mwezi Juni/Julai 2024.

**<u>HITIMISHO</u>**

30. Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika unawakilisha hatua muhimu katika jitihada za Afrika za kujitegemea na kuwa na ufadhili endelevu wa shughuli za kuleta amani na usalama. Kwa kulinganisha na ajenda ya mageuzi ya AU na kupanua wigo wake wa rasilimali zake, Mfuko wa Amani unaweza kuchukua jukumu muhimu katika kuhakikisha kuwa kuna Afrika yenye amani zaidi. Kuendelea kujitolea kwa Nchi Wanachama wa AU kwa kutenga kiasi fulani kutoka kwa Mfuko wa Amani kupitia Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama hadi kwa walengwa husika (nchi wanachama, RECs…) katika bajeti ya 2025 itakuwa mfano halisi wa umiliki wa Afrika na ufadhili endelevu.

**AFRICAN UNION  UNION AFRICAINE**

**African Union Common Repository** **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-02-15

# Report of the Chairperson of the Commission on the Operationalization of the African Union Peace Fund

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10527

*Downloaded from African Union Common Repository*